

Maswali na Majibu

1. Mbona Mungu alipea Waisraeli sheria?
Kuwaonyesha vile alitaka waishi na kuwafanya wawe taifa lake kubwa hapa duniani.
2. Amri 10 ziliwafunza Waisraeli nini?
Vile wanaweza kumpenda na kumtii Mungu. Tena vile wanaweza kuenenda kati yao.
3. Jina la hema la kipekee lenye Waisraeli walitumia kwa kuabudia Mungu liliitwaje?
Maskani.
4. Chumba cha kwanza kwenye hema kiliitwaje? *Pahali Patakatifu.*
5. Nani alikubaliwa kwenda Pahali Patakatifu? *Makuhani.*
6. Vitu gani 3 vilikuwa Pahali Patakatifu?
Kinara cha taa, meza na mkate, madhabahu ya uvumba.
7. Chumba cha pili kwenye Maskani kiliitwaje? *Pahali Patakatifu Sana.*
8. Nani alikubaliwa kwenda Pahali Patakatifu Sana? *Kuhani Mkuu pekee yake.*
9. Kuhani Mkuu alienda huko wakati gani na alifanya nini?
Mara moja kwa mwaka, Siku ya Upatanisho. Aliomba Mungu asamehe watu dhambi.
10. Nini ilikuwa Pahali Patakatifu Sana? *Sanduku*

Mistari ya kukariri

Jifunze amri 10

Mazungumzo

Eleza juu ya Maskani na kila kitu kilichokuwa ndani. Kila kitu kilitumika kwa nini? Tunajifunza nini kwa siku za sasa.

Kuandika

Andika amri 10. Amri gani ndiyo unaona ni ngumu sana kutimiza wakati wa sasa?

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 16 Amri za Mungu


SOMA Kutoka 20:1—17

SOMO

Waisraeli walikuwa watumwa Misri. Waliti wasimamizi wao. Hawakuwa na sheria zao. Walikuwa taifa. Walitakiwa wawe na sheria za kuwafundisha vile wanaweza kuishi pamoja kama jamii. Mungu aliwapa sheria ili wawe taifa lake kubwa hapa duniani. Wakitii amri za Mungu, watakuwa mfano mzuri na kuonyesha watu wengine kwamba wanapenda Mungu na wanamtii.

Taifa la Israeli walipiga kambi chini ya Mlima wa Sinai. Mungu alikumbusha Musa kwamba Waisraeli ni watu wake wakipekee. Mungu aliwachagua kuwa watu wake wakati aliahidi Ibrahimu kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa. Mungu aliahidi kwamba ikiwa taifa la Israeli watampenda na kumtii, atawalinda na kuwaongoza mpaka Nchi ya Ahadi ya Kanaani. Watu hawa waliahidi kwamba watampenda Mungu na kumtii.

Musa alienda juu kwa Mlima wa Sinai na akakaa kule kwa siku 40. Mungu aliwapa Waisraeli sheria zenye walitakiwa wazitii. Mungu alisema kwamba watakuwa watu wake wakipekee. Hizi sheria au amri ziliandikwa kwa mawe yaliyochongwa.



Amri 10 zilikuwa zionyeshe Waisraeli vile Mungu alitaka waishi. Amri chache za kwanza ziliwafundisha vile wanatakiwa wapende na wamtii Mungu. Zilizobaki ziliwafundisha vile wanaweza kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe. Waisraeli waliahidi kwamba watatii hizo amri. Mungu aliahidi kuwalinda ikiwa watatii amri zake.

Amri kumi

1. Mungu ni mmoja. Lazima usiabudu miungu.
2. Lazima usitengeneze sanamu.
3. Lazima usitumie jina la Mungu vibaya .
4. Lazima usitarehe Siku ya Sabato yaani siku moja kwa wiki.
5. Lazima utii wazazi wako na uwalinde.
6. Lazima usiue.
7. Lazima usiwe na ngono inje ya ndoa.
8. Lazima usiibe.
9. Lazima usiseme uongo au usishuhudie uongo kwa wenzako.
10. Lazima usiwe na wivu kwa vitu vya wenzako kwa kutamani.

Mungu aliambia Musa vile wanatakiwa wamuabudu. Mungu alitaka watengeneze mahali pakumwaabudia. Hii ilikuwa hema la kipekee liitwalo *Maskani*. Hii maskani ilitakiwa iwe katikati ya kambi. Waisraeli walikusanya vitu vyote vyenye Wamisri waliwapea: dhahabu, fedha, johari, na nguo za kitani. Hivi vitu vilitumika kutengeneza maskani. Mungu aliwambia vile wataitengeza sawasawa.

Maskani ilikuwa ndani ya ua. Ukuta wa ua ulitengenezwa kwa kitani nyeupe. Kulikuwa na mlango mmoja wa kuingia kwa ua. Ndani yake kulikuwa na bakuli kubwa ya shaba iliyotumika na makuhani kwa kunawa. Kulikuwa na madhabahu ya shaba iliyotumika kwa matoleo ya dhabihu. Maskani ilifundisha watu masomo. Walijifunza vile wanatakiwa waabudu Mungu na hiyo ndiyo ilikuwa njia sahihi pekee. Maskani ilikuwa katikati ya kambi, kwa hivyo walitakiwa waweke Mungu katikati ya maisha yao.

Maskani ni hema iliyokuwa katikati ya ua. Ilikuwa na sehemu mbili: sehemu ya kwanza iliitwa Patakatifu na sehemu ya pili iliitwa pahali Patakatifu Sana. Vyombo vya maskani vilikuwa vya dhahabu.

Makuhani tu, ndiyo walikubaliwa kuingia Pahali Patakatifu. Katika Pahali Patakatifu kulikuwa na kinara ya taa, meza na madhabahu ya kufukizia uvumba.

Mafundisho kwetu

Kuna njia moja tu ya wokovu – kupitia kwa Yesu. Tunatakiwa tuoshwe kwa kubatizwa Lazima Mungu awe katikati ya Maisha yetu

Kinara ya taa ya dhahabu ilikuwa na matawi 7. Iliwaka muda wote. Hii ilionyesha kwamba mwangaza wa wokovu wa Mungu unawaka na kun'gaa wakati wote. Juu ya meza kulikuwa na mikate 12 ya mvingo na laini. Kila wiki waliweka mikate mipya. Hizi mikate 12 (moja kwa kila kabila ya Israeli) kuonyesha kwamba kabila 12 za Israeli walikuwa mbele ya Mungu wakati wote. Uvumba uliwaka juu ya madhabahu ya dhahabu kila asubuhi na jioni. Uvumba huwa unatoa harufu nzuri wakati unawaka. Uvumba ulisimamia maombi ya watu. Maombi inatakiwa iinuliwe juu kama moshi nzuri kwa Mungu.

Mafundisho kwetu

Kinara ya taa – mwanga wa Injili na uwake mioyoni mwetu

Mkate – tusome neno la Mungu, ndiyo mkate wa uzima, itusaidie tuwe karibu na Mungu

Uvumba – maombi yetu iwe na harufu nzuri na iende juu kwa Mungu.

Pahali Patakatifu Sana palikuwa patakatifu na Kuhani Mkuu pekee (kuhani wa maana sana) yake ndiye alikubaliwa kuingia ndani. Alikubaliwa kuingia mara moja tu kwa mwaka. Kuhani mkuu alienda Mahali Patakatifu Sana kuuliza Mungu asamehe watu dhambi zao Siku ya Upatanisho.

Sanduku la dhahabu liliwekwe Pahali Patakatifu Sana. Hapo ndipo Mungu aliishi. Sanduku ilikuwa takatifu sana. Kwa hiyo sanduku ndio uwepo wa Mungu ulikaa. Sanduku ilikuwa ya mbao na kufunikwa kwa dhahabu. Kulikuwa na makerubi mbili kwa kifuniko. Kifuniko katikati ya makerubi kiliitwa Kiti cha Rehema. Hapo ndipo rehema na upendo wa Mungu ulikuwa. Ndani ya Sanduku kuliwekwa mawe ya amri 10 na chungu cha mana. Mtu yeyote hakukubaliwa kushika hilo Sanduku – au akufe. Sanduku lilibebwa na makuhani wanne juu ya miti mbili wakati wa kuhama.

Haruni nduguye Musa na wanawe ndio walitakiwa wawe makuhani. Ndio walikuwa wafundishe watu juu ya Mungu. Mungu aliwaagiza Waisraeli wamtotee dhabihu za wanyama. Walichifunza kwamba lazima dhambi zao zinasamehewe tu kwa kuchinja mnyama. Kumbuka, wakati Adamu alifanya dhambi kwa Bustani ya Edeni, adhabu yake ilikuwa kifo. Kwa hivyo kila mtu aliyefanya dhambi, adhabu yake ilikuwa kifo. Lakini Mungu alikuwa mzuri na huruma akawambia wakichinja mnyama kuonyesha kwamba wanasikitikia dhambi zao, Mungu aliwasamehe.

Fundisho kwetu

Yesu alikufa na akafufuka tena ili Mungu atusamehe dhambi zetu tukitubu.